# STD 4 END TERM 3 EXAM 2019

## KISWAHILI

***Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Jaza kila pengo kwa kuchagua jawabu lifaalo zaidi.***

Fatuma na Amina ni ___1___ wanaopendana kama chanda na ___2___. Wana umri ___3___ miaka ___4___. Wao hutafutana kila ___5___ wakitoka shuleni ___6___ wanasomea shule tofauti. Kitu ___7___ cha Fatuma ___8___ cha Amina na ___9___ cha Amina hutumiwa na Fatuma. Watoto hawa wamependana ___10___ walipohamia ___11___ wa Tumaini. Tabia ___12___ ni zile ___13___ wazazi wengi ___14___. Bila shaka, watakuwa na maisha ___15___ baadaye.


| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. waschana | B. wabinti | C. wasichana | D. wavulana |
| **2.** | A. pede | B. bete | C. upote | D. pete |
| **3.** | A. wa | B. ya | C. la | D. na |
| **4.** | A. nane | B. mikumi | C. tano | D. minane |
| **5.** | A. alfajiri | B. adhuhuri | C. asubuhi | D. jioni |
| **6.** | A. maana | B. kwasababu | C. kwa sababu | D. kwa |
| **7.** | A. lolote | B. chochote | C. yoyote | D. zozote |
| **8.** | A. huwa | B. kitakuwa | C. kinakuwa | D. kimekuwa |
| **9.** | A. ule | B. kile | C. ile | D. zile |
| **10.** | A. tena | B. hata | C. tangu | D. hadi |
| **11.** | A. miji | B. kijiji | C. mtaa | D. nchi |
| **12.** | A. zao | B. wao | C. yao | D. vyao |
| **13.** | A. ambaye | B. ambayo | C. ambao | D. ambazo |
| **14.** | A. huchukia | B. hudharau | C. hukemea | D. husifia |
| **15.** | A. njema | B. mema | C. mzuri | D. vizuri |

**Kuanzia swali la 16-30, chagua jibu sahihi kulingana na maagizo uliyopewa.**

16. Chagua sentensi iliyo na kiulizi '**-pi**'.
    A. Mbona hukujibu maswali yote?
    B. Tutaenda kwenu lini?
    C. Maji ya kunywewa ni yapi?
    D. Ni nani aliyebisha?

17. Mwalimu hufundisha na daktari
    A. hudunga  B. huendesha
    C. hutibu  D. huponya

18. Umbo hili huitwaje?



    A. Pia
    B. Duara
    C. Mraba
    D. Mche duara

19. Neno '**gari**' huwekwa katika ngeli ya
    A. KI-VI  B. A- WA
    C. I-ZI  D. LI- YA.

20. **Andika kwa wingi;**
    Paka wangu ana njaa.
    A. Paka zangu zina njaa.
    B. Paka wangu wana njaa.
    C. Paka wetu wana njaa.
    D. Mapaka yetu yana njaa.

21. Utamwitaje kaka wa baba yako?
    A. Mjomba.  B. Halati.
    C. Amu.  D. Babu.

22. Chagua sentensi iliyotumia kiashiria vizuri.
    A. Chakula hii ni tamu.
    B. Yai lile ni kubwa.
    C. Nyati hii itakuumiza.
    D. Baraka alidungwa na misumari hizo.

23. Tunasema mfupi kama nyundo na mkali kama
    A. simba  B. moshi
    C. askari  D. sungura.

24. Bwana Sumba amevalia shati
    A. weupe  B. meupe
    C. nyeupe  D. jeupe.

25. Chagua kitenzi kilicho katika wakati unaofaa.
    A. Watasoma- uliopo.
    B. Nimekuja- timilifu.
    C. Anaimba- mazoea.
    D. Ilinyesha- ujao.

26. Chagua jibu lenye vokali pekee.
    A. z, b, d, l
    B. ch, dh, gh
    C. a,e,i, o, u
    D. t, f, h, l

27. Mkokoteni ____ na punda.
    A. huvutwa
    B. hufutwa
    C. huvurutwa
    D. hufuratwa

28. Ukiwa wa mwisho **<u>usikate tamaa.</u>** Maneno yaliyopigwa mstari yanamaanisha
    A. usipoteze matumaini
    B. usitarajie mema
    C. ufanye bidii
    D. uonyeshe wivu.

29. Saa mbili zina dakika ngapi?
    A. Ishirini.
    B. Mia moja na ishirini.
    C. Mia mbili.
    D. Sitini.

30. Haba na haba hujaza kibaba. Huu ni mfano wa
    A. tashbihi
    B. kitendawili
    C. semi
    D. methali.

Compiled & distributed by Schools Net Kenya, P.O. Box 15509-00503, Mbagathi –Nairobi | Tel:+254202319748E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

***Soma ufahamu huu kisha ujibu maswali 31-40.***

Kuna watu wengi wanaovaa nguo zinazofanana. Nguo kama hizi huitwa sare. Baadhi ya wale ambao huvaa sare ni wanajeshi, askari na wanafunzi shuleni. Je, umewahi kujiuliza kwa nini wanafunzi huvaa sare?

Sababu ya kwanza ni kujitambulisha. Ni rahisi kujua shule ya mwanafunzi aliye katika sare. Sare nyingine huwa na majina ya shule hasa kwenye mifuko. Shule nyingi zinapokutana katika michezo hutambuliwa kwa sare. Hebu fikiria itakavyokuwa ikiwa kila mwanafunzi atavaa nguo za nyumbani.

Pia, sare huwafanya wanafunzi kuwa salama. Iwapo mtoto atapotea akiwa katika sare, itakuwa rahisi kuwapata wazazi. Atapelekwa katika shule anayosomea ili wazazi waarifiwe. Zipo sababu nyingi za kuvaa sare na kila mwanafunzi anafaa kuipenda ya shule yake.

**31.** Nguo zinazofanana huvaliwa na watu
A. wachache
B. kadhaa
C. wengi
D. wote.

**32.** Nguo zinazofanana huitwa
A. jezi
B. shati
C. aproni
D. sare.

**33.** Ni watu gani ambao hawakutajwa kuvalia sare?
A. Walimu.
B. Wanafunzi.
C. Wanajeshi.
D. Askari.

**34.** Mwandishi ametaja sababu ngapi za kuvaa sare?
A. Mbili
B. Moja
C. Tatu
D. Nne

**35.** Mwanafunzi akiwa katika sare ya shule
A. huelewa vizuri
B. hupotea haraka
C. hawezi kuwa mtundu
D. hutambulika kwa urahisi.

**36.** Sare nyingine huwa na majina ya shule kwenye
A. suruali
B. mifuko
C. mgongo
D. ukosi.

**37.** Nguo za nyumbani
A. hufanana
B. hazitawatambulisha wanafunzi vilivyo
C. hupendeza kuliko sare za shule
D. hutambulisha wanafunzi kwa urahisi.

**38.** Ipi si faida ya sare?
A. Kuwafanya wanafunzi wawe werevu.
B. Kutambulisha wanafunzi.
C. Kufanya wanafunzi wawe salama.
D. Kujua shule ya mwanafunzi.

**39.** Shule nyingi huweza kukutana wakati wa
A. vita
B. kusoma
C. michezo
D. kupima sare.

**40.** Unafaa kuipenda shule yako kwa sababu
A. kila mwanafunzi huvaa sare
B. imejengwa vizuri
C. inakuwezesha kupata elimu
D. inakuwezesha kuvaa sare.

**_Soma ufahamu huu kasha ujibu maswali 41-50._**

Chavu alipomwona Chaurembo na vipuli masikioni aliingiwa na wivu. Alitaka naye atoboe masikio yake na kutia mapambo mazuri zaidi. Alimwendea mama yake na kumwambia apelekwe kwenye duka la mapambo ili atobolewe masikio. Mama aliposema hana pesa, Chavu aliangua kilio hadi akaahidiwa kupelekwa.

Alipopelekwa alihisi uchungu mwingi lakini akavumilia. Alianza kutibu mashimo kwenye masikio ili yapone. Badala yake, masikio yake yalianza kuvimba. Juma lilipoisha, sikio lilikuwa na uvimbe mkubwa kama embe zima. Ilibidi apelekwe hospitalini ili uvimbe uondoke lakini sehemu ya chini ya sikio ilikatwa pia.

**41.** Chaurembo alikuwa na
- A. wivu
- B. vipuli masikioni
- C. uvimbe
- D. upendo.

**42.** Chavu alitaka masikio yake yafanyweje?
- A. Yatibiwe.
- B. Yakatwe.
- C. Yaondolewe.
- D. Yatobolewe.

**43.** Chavu alitiwa mashimo masikioni wapi?
- A. Shule ya msingi
- B. Hospitalini
- C. Duka la mapambo
- D. Kiwanda cha masikio.

**44.** Chavu alianza kulia kwa sababu
- A. aliadhibiwa
- B. aliambiwa kuwa pesa hazikuwepo
- C. alihisi uchungu mwingi
- D. masikio yalivimba.

**45.** Chagua sentensi sahihi.
- A. Masikio ya Chavu hayakutobolewa.
- B. Chavu alimpenda Chaurembo.
- C. Chavu alitaka kuweka mapambo masikioni.
- D. Chaurembo na Chavu walikuwa ndugu.

**46.** Kilio cha Chavu kilimfaa kwa sababu
- A. aliahidiwa kutobolewa masikio
- B. mama alimnyamazisha
- C. aliletewa vipuli
- D. masikio yalipona.

**47.** Siku saba zilipoisha
- A. sikio lilikuwa limevimba zaidi
- B. uvimbe ulikuwa umeisha
- C. sikio lilivimba kidogo tu
- D. mapambo yalitiwa sikioni.

**48.** Tunaambiwa kwamba sikio lilibadilika na kuwa kama
- A. nyama
- B. embe
- C. mpira
- D. vipuli.

**49.** Chavu alifanyiwa nini hospitalini?
- A. Alipewa mapambo ya masikio.
- B. Alikatwa sehemu ya chini ya sikio.
- C. Alikatwa masikio yote.
- D. Alitobolewa masikio.

**50.** Kutokana na kisa hiki tunajifunza kuwa
- A. tusitie vipuli masikioni
- B. masikio huua
- C. mapambo ni muhimu
- D. wivu haufai.